

**Chanzo>> Wamasai wanadaiwa kwenda kupora mifugo**

# Mmoja auawa, wanne wajeruhiwa mapigano baina ya wafugaji Kilosa

Na LATIFA GANZEL, Morogoro

**M**TU mmoja amefariki dunia na wengine wanne wajeruhiwa, baada vurugu zilizoibuka katika Kijiji cha Tindiga, Tarafa ya Masanze, Wilayani Kilosa, baina ya wafugaji wa jamii ya Kimasai na wale wa jamii ya Kisukuma.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki, saa 12 jioni, baada ya mvutano wa wafugaji wa Kimasai, kutaka kuchukua kwa nguvu mifugo ya mfugaji wa Kisukuma, na kusababisha vurugu, ambapo John Nyerere, alifariki dunia.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, akiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, walifika katika kijiji hicho, akawasihi wananchi kuwa watulivu wakati vyombo vya dola

vikifuatilia na kuchukua hatua dhidi ya watuhumiwa waliohusika na mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim, alisema kwa taarifa zilizoripotiwa polisi, chanzo cha vurugu hizo ni kundi la wamasai lililokwenda kuiba ng'ombe kwa jamiil ya kisukuma na wakati wanawaswaga, ndipo yakatokea mapigano.

Muslim alisema watu 19, wanatafutwa kwa tuhuma za kuhusika katikavurugu hizonawatakopamatwa, watafikishwa mahakamani.

Mkazi wa Kijiji cha Tindiga, Said Kindamba, alisema wafugaji wametawala katika maeneo hayo na kwamba, kesi zimekuwa zikiripotiwa, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa na kuwaomba viongozi kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika.

Naye, Mkazi wa Tindiga, Mohamed Msilimu, alisema kumekuwa na vurugu za muda mrefu katika eneo hilo, lakini kutokana na kufumbiwa macho na baadhi ya viongozi waliopita, kumesababisha mapigano.

Alisema vurugu siyo kwa wafugaji wenyewe pekee, bali hata wakulima na wafugaji, zimekuwa zikitokea kutokana na mashamba yao kulishwa mifugo, hususan kipindi cha kilimo.

Katika hatua nyingine, Shigela aliagiza kukamatwa kwa Nassoro Nzige, ambaye ni kinara wa kupanga njama na wafugaji kulisha mifugo katika mazao ya wakulima.

Shigela alisema mwananchi huyo na wenzake, wamekuwa wakipanga njama kwa kupita mashambani na baadae kwenda kwa wafugaji kupewa fedha na nyingine kuwapatia askari polisi.